**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOSA**

SHULE YA SEKONDARI MAZINYUNGU,
S.L.P. 139,
**KILOSA.**
TAREHE: ..............................

**Kumb. Na.** MSS/JOIN/VOL.II/2021
JINA LA MWANAFUNZI........................................................

SHULE YA MSINGI......................................... ...........

**KILOSA.**

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATOCHA KWANZA SHULE YA SEKONDARI MAZINYUNGU WILAYANI KILOSA MKOANI MOROGORO MWAKA 2021.**

## 1.0 UTANGULIZI:

Ninafurahi kukuarifu kwamba umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika Shule ya Sekondari Mazinyungu Mwaka 2021. Shule ipo umbali wa km 2 kutoka **Mamlaka ya mji mdogo wa Kilosa**.

Zoezi la usajili kwa wanafunzi wa kidato cha kwanza litaanza rasmi siku ya Jumatatu tarehe **04/01/2021** kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 7:00 Mchana, tayari kwa kuanza masomo ya Mhula wa kwanza siku ya Jumatatu tarehe **11/01/2021**. Mwisho wa kuripoti ni tarehe **15/1/2021.**

## 2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:

### 2.1 SARE ZA WANAFUNZI.

**WAVULANA**

Suruali 2 mpya, rangi ilionyeshwa katika kitambaa ( bluu bahari iliyoiva) marinda manne madogo mbele ambapo kushoto mawili na kulia mawili, mifuko miwili ya mbele ya kawaida kushoto mmoja na kulia mmoja, mfuko mmoja wa nyuma kulia,iwe siyo ya kubana yenye luksi za kawaida ( siyo pana ) na pindo kubwa la nje miguuni (turn up) na upana wa suruali kwa chini iwe kuanzia 15 hadi 16 Inchi.

Scanned with CamScanner

Mashati mapya mawili marefu kwenda chini yenye kola , mikono mifupi, mfuko mmoja ,yasiyobana na liwe na alama ya kidato cha kwanza begani.

Viatu vipya vyeusi vya ngozi, kisigino kifupi na soksi nyeupe fupi zisizo na pambo lolote.

Sweta jipya lenye mikono mirefu na rangi inayofanana na sketi au suruali ya shule.

**WASICHANA**

Sketi mpya 2, rangi iliyoonyeshwa katika kitambaa (bluu bahari – iliyoiva).
Marinda boksi mawili makubwa **1** mbele katikati na **1** nyuma kisha marinda 3 ya kawaida baada ya rinda kubwa mbele na nyuma kushoto na kulia , fika shuleni kwa mfano zaidi.

Mashati mawili, marefu yenye kola, mikono mifupi , mfuko mmoja na yasiyobana fika shuleni kwa mfano.

Sweta lenye mikono mirefu na rangi inayofanana na sketi au suruali ya shule ( ukipenda). Hata hivyo wasichana wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu badala ya shati kwa wanaoishi misingi hiyo.Hijabu husika iwe yenye nusu kanzu na si vinginevyo.

**NB:** siku ya Jumatano na Ijumaa wanafunzi huvaa tsheti ya **dark** bluu yenye nembo ya shule, aidha shati huvaliwa na tai ambapo upatikanaji wa tai na tsheti huratibiwa na idara ya Malezi na nidhamu.
**Inasisitizwa sana** utaratibu wa sare kufuatwa, Kinyume na maagizo hayo, mwanao atarudishwa ili umshonee sare nyingine. Kama fomu hii inavyoagiza rangi na vipimo vyake.

**SARE ZA MICHEZO:**

Mwanafunzi anatakiwa kuwa na jezi za michezo zenye rangi ya bluu kwa kujinunulia mwenyewe kwa ajili ya siku za michezo hapa Shuleni.

## 2.2 VIFAA VYA DARASANI NA USAFI WA MAZINGIRA:

Mwanafunzi anatakiwa kuja shuleni na Daftari kubwa 12, kalamu za kutosha, Rula moja kubwa, Penseli na Mkebe wa Hesabu mmoja.
Kila Mwanafunzi aje na Jembe **1** na mpini wake, fyekeo 1, na mfagio wa nje aina ya Chelewa uliofungwa kwenye mti wake., kwa ajili ya shughuli za usafi wa mazingira ya Shule.

## 2.3 CHAKULA CHA WANAFUNZI:

Shule hii hutoa chakula cha mchana ili kumwezesha mwanafunzi kumudu masomo yake vyema kwa kushirikiana na mzazi/mlezi.
Mwanafunzi anatakiwa kuja na yafuatayo kwa ajili ya chakula cha muhula mmoja:

1) Mchele Kg 12. Ambapo atakula wali mara mbili kwa wiki.
2) Maharage Kg 5. Kwa ajili ya wali na makande.
3) Pesa tasilimu Tsh. 5,000. Kwa ajili ya wapishi, mafuta, viungo na uendeshaji.
4) Chenga za mahindi kg 15.



Scanned with CamScanner

## 2.4 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule hii inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na. 10 ya Mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Rais –**TAMISEMI** yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji elimu.

Aidha unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

a) Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wenzako na jamii inayokuzunguka kwa ujumla.
b) Mahudhurio mazuri kwa kila Shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya Shule.
c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni **(Preparation)**.
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili, mavazi, na mazingira ya Shule.
g) Kuvaa sare za Shule wakati wote unapotakiwa.
h) Kuzingatia ratiba ya Shule wakati wote na
i) Kutunza mali za umma.

## 2.5 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji, ushoga, na kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi.
3. Ulevi wa aina yoyote.
4. Uvutaji wa sigara, matumizi ya madawa ya kulevya na matumizi ya mirungi.
5. Makosa ya jinai (mwanafunzi akithibitika kutenda kosa la jinai, kuhukumiwa kifungo).
6. Kupiga au kupigana.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma/kutotunza mali ya umma (mfano kuninginia kwenye grill kuvunja madawati, kuchora kuta, kupoteza mali alizokabidhiwa mfano slesha, majembe, madumu nk.
8. Kudharau mbendera ya Taifa.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba, kutoa mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
11. Kutoroka shule kabla ya wakati.
12. Kuchelewa na kutoripoti au kuwahi kufunga Shule.
13. Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo au kuvuruga amani na usalama wa watu.
14. Kukataa adhabu kwa makusudi.
15. Kukaa chaka/porini.
16. Kuchora michoro kwenye kuta za majengo na kuandika **matusi.**



Scanned with CamScanner

## 2.6 MAKOSA YAFUATAYO YATASABABISHA MWANAFUNZI KUPEWA ADHABU KALI

Mfano wa adhabu kali inaweza kuwa viboko visivyozidi vinne (4), kazi za mazingira na kusimamishwa Shule na marudio ya makosa yatasababisha mwanafunzi kuachishwa masomo kwa makosa yafuatayo;

1. Kutovaa mavazi rasmi ya Shule.
   Mwanafunzi ni lazima awe katika mavazi rasmi ya Shule muda wote awapo Shuleni.
   a) Siku za masomo tangu asubuhi hadi mwisho wa vipindi vya masomo.
   b) Wakati wote wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za kishule kama mikutano, matibabu, safari, michezo, remedial/masomo ya jioni.
2. kujipamba akiwa shuleni kama kupaka wanja, hina, manukato, kuvaa hereni, kutinda nyusi, kupaka kucha rangi, kujichubua nk.
3. kunyoa **KIPARA**, kuvaa nguo zenye mtindo wa **LEGEZA** na mitindo mingine ya kihuni. Wanafunzi wa kiume hawaruhusiwi kufuga ndevu, kadhalika na mwanafunzi wa kike haruhusiwi kusuka.
4. kutumia dawa za kubadili nywele au kubadili rangi ya ngozi.
5. kuvaa nguo zisizokuwa na heshima.
6. Kwenda nyumbani kwa mwalimu/mtumishi bila ruhusa ya utawal wa Shule.
7. Kuandika katika vitabu vya shule, kuta, madawati,viti, meza na ubao wa kufundishia bila kuwa na kibali.
8. Kutumia lugha ya matusi shuleni.
9. Kutoshiriki katika kazi za mikono shuleni (tatizo la kiafya liwasilishwe.kwa mkuu wa shule likiwa na uthibitisho wa daktari).
10. Kutohudhuria vipindi na masomo ya dini yake.
11. Kutotii viongozi wa ngazi mbalimbali.
12. Kutoishi na kushirikiana kidugu.
13. Kufanya biashara katika eneo la shule bila kibali.
14. Kuonekana katika nyumba za wageni (Guest House) na nyumba za starehe kama vilabu vya Pombe.

## 2.7 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASHWA KUKAMILISHWA.

a) Medical examination form ambayo itajazwa na Mganga wa Hospital ya Serikali. Fomu hii itakabidhiwa kwa Mkuu wa Shule mara utakaporipoti Shuleni.
b) Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
c) Fomu ya mzazi kikiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotoleawa na Shule.

**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII.**

..........................

***Ngamba M. Manegese,***

**MKUU WA SHULE**
**0658-240086**

MAZINYUNGU SECONDARY SCHOOL
HEADMASTER
18 DEC 2020
P.O. Box 139, KILOSA



Scanned with CamScanner

## HATI YA UTII WA SHERIA ZA SHULE

**SEHEMU A" (IJAZWE NA MZAZI /MLEZI).**

Mimi Bwana/ Bibi/Bi.......................................................................................

Mzazi /Mlezi wa ...........................................................................

Nimesoma kwa makini sheria za Shule kama zilivyoandikwa katika barua hiii yenye **Kumb. Na.** MSS/JOIN/VOL.II/2020 ya tarehe........................

Ninazikubali sheria hizo na nitashirikiana na uongozi wa Shule kuona kuwa mwanangu................................................anazifuata kwa manufaa yake na kwa manufaa ya umma.

**SEHEMU B" (IJAZWE NA MWANAFUNZI).**

Mimi....................................................

Mtoto wa Bwana/Bibi/Bi......................................................

Mbele ya Baba/Mama/mlezi...................................................

Ninakiri kwamba nimesoma kwa makini sheri za Shule kama zilivyoandikwa katika barua hii yenye **Kumb. Na.** MSS/JOIN/VOL.II/......................ya tarehe......................

Ninakubali sheria hizo nitazifuata na kuzitii kuwa ninaelimishwa na umma kwa manufaa yangu na manufaa ya umma.

.................................. **SAHIHI YA MWANAFUNZI**
TAREHE..............................

............................................ **SAHIHI YA MZAZI/MLEZI**
TAREHE........................

(Hati hii ijazwe kisha irudishwe kwa Mkuu wa Shule)



Scanned with CamScanner

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

PRESIDENT'S OFFICE
REGIONAL ADMNISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT
KILOSA DISTRICT COUNCIL

**FORM NUMBER 1.**

**TO THE MEDICAL OFFICER**

…………………………………………………
…………………………………………………
…………………………………………………

**RE: REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION TO:** ……………………………………………………

Please examine the above named pupil and give us the report regarding his/her suitability for undertaking secondary School students.

1.Blood……………………………………………………………………………………………

2.Stool……………………………………………………………………………………………

3.T.B. Test…………………………………………………………………………………………

4.Syphilis Test……………………………………………………………………………………

5.Urine Examination………………………………………………………………………………

6.Eye Test…………………………………………………………………………………………

7.Chest Test………………………………………………………………………………………

8.Ears Test…………………………………………………………………………………………

9.Spleen……………………………………………………………………………………………

10.Abdomen…………………………………………………………………………………………

11.Pregnancy………………………………………………………………………………………

**ANY ADDITIONAL INFORMATION**:eg.Physical defect or impairment and family diseases……………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

I Certify that ,the above pupil is suitable/ unsuitable for Secondary School students.If unsuitable give reasona,
……………………………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………………………

**Name of the Medical officer** :…………………………………………………………Signature………………………

Date……………………………………………… Official Stamp:

Scanned with CamScanner